# HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA
# MUHTASARI WA KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI
# KILICHOFANYIKA TAREHE 28-29/04/2016

**MAHUDHURIO**

| | | |
|---|---|---|
| **1.** | MH. ERICK E. NKILAMACHUMU | MWENYEKITI |
| **2.** | BW. KEVIN S. MAKONDA | KATIBU (DED) |
| 3. | MH.JOHN M. SHIMI I'MANA | MJUMBE |
| 4. | MH.MKUBILA S. SOUD | MJUMBE |
| 5. | MH.ADRONIZI E. BURINDOLI | MJUMBE |
| 6. | MH.OLIPA A. BUGOKE | MJUMBE |
| 7. | MH.KHAMIS B. HAMADI | MJUMBE |
| 8. | MH.ROMAN MITABARO | MJUMBE |
| 9. | MH.JUSTUS K. MASUMO | MJUMBE |
| 10. | MH.DAVID I BUZUTU | MJUMBE |
| 11. | MH.GWIHANGWE M. EDWARD | MJUMBE |
| 12. | MH. VAILETH MADENDE | MJUMBE |
| 13. | MH.SAID R. SOUD | MJUMBE |
| 14. | MH.ZAWADI A. COSMAS | MJUMBE |
| 15. | MH.WILBARD J.BAMBARA | MJUMBE |
| 16. | MH.GWASSA NTUNGIYE | MJUMBE |
| 17. | MH. SUZANA BAHATI | MJUMBE |
| 18. | MH. FIDEL F. NDANGWA | MJUMBE |
| 19. | MH.MUKIZA S. BYAMUNGU | MJUMBE |
| 20. | MH.NZEYE LEONARD | MJUMBE |
| 21. | MH.SENTORE J. MIBURO | MJUMBE |
| 22. | MH.PHILBERT M KIIZA | MJUMBE |
| 23. | MH.MUGATA M. ELIAS | MJUMBE |
| 24. | MH.GEORGIA MUNYONYELA | MJUMBE |
| 25. | MH.KAGOMBA S. GEORGE | MJUMBE |
| 26. | MH.LAURENT J. MUSUNGARERE | MJUMBE |
| 27. | MH.CATHERINE EDWARD | MJUMBE |
| 28. | MH.REHEMA S. RAMADHANI | MJUMBE |
| 29. | MH.SAFARI N. BANIGWA | MJUMBE |
| 30. | MH. EDITHA MWINURA | MJUMBE |
| 31. | MH ALEX GASHAZA(MB) | MJUMBE |

**WAJUMBE WAALIKWA**

| | | |
|---|---|---|
| **1.** | BI. HONORATHA CHITANDA | MKUU WA WILAYA |
| 2. | BW. ELIAS ZEPHANIA | MWANDISHI WA HABARI, RK |
| 3. | BW. HUDSON BAGEGE | MWENYEKITI- CCM(W) |
| 4. | BW. JACOB MAKUNE | KATIBU- CCM (W) |

**WATAALAM WALIOHUDHURIA:**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | BW. BIGAMBO AMOS | AFISA MIPANGO (W) |
| 2. | BW. MASOUD ABDALLAH | MWEKA HAZINA(W) |
| 3. | BW. MOSES KICHOGO | AFISA HABARI |
| 4. | BW. BULILO MUSOMBWA DEYA | MWANASHERIA WA (W) |
| 5. | BW. F.M KAPAMA | MKAGUZI WA NDANI(W) |
| 6. | BW. JUMANNE MAGUNGU | KAIMU MUHANDISI WA MAJI |
| 7. | BW. JULIUS ERNEST | KNY AFISA TARAFA NYAMIHAGA |
| 8. | BW. THEONEST THADEO | KAIMU AFISA TARAFA KANAZI |
| 9. | BW. MORIS MOMBIA | KAIMU AFISA TARAFA RULENGE |
| 10. | BW. PASTORY M. MSABILA | AFSA TARAFA MURUSAGAMBA |
| 11. | BW. CONSTANTINE MUDENDE | KAIMU AFISA KILIMO WILAYA |
| 12. | BW. FIDELIS MALIMBU | K/AFISA ELIMU SEKONDARI(W) |
| 13. | BW. SANGATATI JOSEPHAT | K/AFISA MIFUGO NA UVUVI(W) |
| 14. | BI. SAKINA CHAMITI | MRATIBU WA TASAF |
| 15. | BW. HERMAN HUME | AFISA MAENDELEO YA JAMII(W) |
| 16. | BI. PERPETUA RULIMBIYE | KAIMU AFISA UGAVI (W) |
| 17. | BW. GIDEON MWESIGA | AFISAELIMU YA MSINGI(W) |
| 18. | BI. BETTY S. MUNUO | AFISA ARDHI(W) |
| 19. | BW. SERIALIS ANTONY | TEO-RULENGE |
| 20. | BW. TOBA A. MUHINA | AFISA MAZINGIRA(W) |
| 21. | BW. STEPHANO NGULINZIRA | AFISA MABORESHO |
| 22. | BW. NELSON RUFANO | KAIMU MGANGA MKUU(W) |
| 23. | BW. FREDRICK KAKURU | KAIMU AFISA UTUMISHI(W) |
| 24. | BW. MICHAEL NDYAMUKAMA | KATIBU TSD(W) |
| 25. | BI. BETTY S. MUNUO | AFISA ARDHI NA MALIASILI (W) |
| 26. | BW. SABUNI S. KASUBI | KAIMU MUHANDISI UJENZI(W) |
| 27. | BI. REINFRIDA ANZIGARY | KATIBU WA KAMATI (H/W) |

**MUHT NA 19/2015/2016: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua kikao kwa kuwasalimia wajumbe, aliwaomba wajumbe kuchangia bila kuvutana kwa sababu miradi mingi ya maendeleo haijatekelezwa hivyo panapohitaji ufafanuzi basi wajumbe watapewa muda kufafanua. Kikao kilifunguliwa saa 5.20 asubuhi

**MUHT NA 20/2015/2016: KURIDHIA AGENDA**

Katibu aliwasilisha agenda, Mjumbe mmoja alisema kwamba iongezwe agenda ya maswali ya papo kwa papo. Wajumbe walijadili na kupokea agenda.

**MUHT NA 21/2015/2016: TAARIFA ZA KATA**

**KATA YA BUKIRIRO**

Kata ya Bukiriro imeundwa na vijiji 4, ina kaya 5048 na watu wapatao 21713 kati yao wanaume 10589 na wanawake 11124, Kigografia upande wa kaskazini inapakana na Kata ya Muganza, magharibi inapakana na Kata ya Rulenge, Kusini inapakana na Kata ya Kabanga na Mashariki inapakana nan chi jirani ya Burundi

Vikao vya ulinzi na usalama vilifanyika 3, Vikao vya ulinzi na usalama vilifanyika kwa 100%, vikao vya VDC vilifanyika kwa asilimia 70%, Mikutano mikuu ilifanyika kwa asilimia 100% kwa vijiji vyote vilivyoko katani, kwa kata ya Bukiriro vikao vya ulinzi na usalama vilifanyika vyote kwa 100%, vikao vya Kamati za maendeleo ya kata WDC vilifanyika vyote sawa 100%.

Utekelezaji wa miradi ya Maendeleo, utengenezaji wa barabara umefikia hatua ya kuzibua mitaro, Mradi wa TASAF III kunusuru kaya maskini 145 fedha ilitolewa kuwapa maskini jumla ya Tshs. 8,811,066.75 kwa kaya 137 kwa kijiji cha Murulama, Mumuhamba mradi wa TASAF III fedha ilitolewa kwa kaya 137 ilikuwa Tshs. 14,381,135.00, kwa kijiji cha Nyabihanga mradi wa TASAF III fedha iliyotolewa ilikuwa ni Tshs. 4,42,454.55/= kwa kaya 125

Kata ina upungufu wa nyumba za waalimu wa shule za msingi, madarasa, madawati meza, viti, kabati na vyoo

Idadi ya wanafunzi walioko katika shule ya msingi wavulana 2143 na wasichana 1959 jumla 4002, Idadi ya wanafunzi katika shule ya sekondari Bukiriro, wavulana 131 na wasichana 128 jumla 259.

Fedha za ruzuku katika shule za msingi, Bukiriro mapato Tshs.534,338.79 hakuna matumizi yaliyofanyika, Rubanga Tshs. 739,930.05 matumizi Tshs. 574,400/= salio lililobaki Tshs. Tshs. 293,930.05, Nyabihanga Tshs. 823,798.41 matumizi Tshs. 468,600/= salio lililobaki Tshs. 355,198.41, Mumuhamba Tshs. 924,189.69/= matumizi Tshs. 375,700./= salio lililobaki Tshs.548,489.69/=, Mubwilinde Tshs. 990,667.54/= matumizi Tshs.379,000/= salio lililobaki ni Tshs. 611,667.54/=, Kigarama Tshs. 1,986,310.00 matumizi Tshs. 1,129,500/= salio lililobaki Tshs. 856,810.99, Rulama Tshs. 1,580,461.29 matumizi Tshs. 635,200/= salio lililobaki ni Tshs. 697,461.29

Fedha za ruzuku shule ya sekondari Bukiriro mapato yalikuwa Tshs. 2,746,000/= hakuna matumizi yaliyofanyika.

Mapato yaliyotokana na zahanati ya Bukiriro H/C salio lilikuwa Tshs. 2,558,000/= matumizi 1,990,800 salio lililobaki lilikuwa ni Tshs. 1,924,345/= mapato yaliyowasilishwa Halmashauri ushuru wa soko Bukiriro Tshs. 500,000/= Ruyigi Tshs. 397,000/=

**KATA YA RUSUMO**
Kata ya Rusumo ina shule za sekondari 2, moja ya Serikali na nyingine ya binafsi, Rusumo B na Baramba Sekondari, Ina zahanati 2, mshikamano na Kasharazi zote ni za serikali na shule za msingi 4, Kabulanzwiri, Rusumo, magereza, na Nyakahanga zote ni za Serikali.

Fedha zilizopokelewa katika robo ya III, Rusumo B sekondari Tshs. 1,991,000/=, zilizotumika 1,329,000/= na kubaki 662,000/=, Fedha zilizopokelewa katika shule za msingi jumla ni Tshs. 2,601,000/= zote hazijatumika

Watumishi walioko katika kata, Elimu msingi waalimu wanaume 29, wanawake 18 jumla 47, Shule za sekondari waalimu wanaume 5, wanawake 3 jumla 8, watumishi wa afya wanaume 1, wanawake 4 jumla 5, watumishi wa kilimo mwanaume 1 na mwanamke 1, Utawala na Utumishi wanaume 4 jumla 4, Shule ya sekondari Bambara waalimu wanaume 6 wanawake 6 jumla 12.

Hali ya mtandao wa maji katika kata ya Rusumo, Kata ina jumla ya vitongoji 13, hivyo vitongoji 9 tu ndivyo vyenye mtandao wa maji ingawa kuna mtandao wa maji.

Hali ya maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi kuna jumla ya wagonjwa 45 ambao tayari walishajikubali sawa na asilimia 0.002 na wote wanapata huduma ya matibabu katika zahanati za katana kituo cha afya Lukole

Vikao vya kisheria vilivyofanyika, Kamati ya Maendeleo ya kijiji kilifanyika kikao 1, kikao 1 bado hakijafanyika, Hlmashauri ya kijiji cha Rusumo hawajafanya kikao, Halmashauri ya kijiji cha kasharazi hawajafanya kikao, mikutano mikuu ya kijiji cha Rusumo ulifanyika mkutano 1 tu, Kijiji cha Kasharazi ulifanyika mkutano 1, Halmashuri ya kijiji cha mshikamano vilifanyika vikao 3, Mikutano mukuu katika kijiji cha mshikamao haikufanyika.

Utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ujenzi wa vyoo katika shule ya msingi Kasharazi umefikia hatua ya kuezeka, shule ya msingi Kablanzwili umekamilika, Rusumo magereza umekamilika, Nyakahanga bado milango.

Shughuli za kiuchumi, wakazi wanajishughulisha na kilimo, biashara, usafirishaji na ufugaji

Hali ya ulinzi na usalama ni nzuri kwani viongozi wanafanya kazi kwa ushirikiano
Changamoto zilizopo katani, Wananchi kutopata maji safi na salama, zahanati ya mshikamao kutokuwa na Mganga Mfawidhi, Utoro kwa wanafunzi kutokana na shule kuwa mbali na maeneo wanayoishi

Maombi maalumu, kutengeneza barabara ya Kasharazi-Rusumo magereza kwa kiwango cha changarawe, ujenzi wa shule moja angalau vyumba 2 katika kitongoji cha Nyamikono

**KATA YA MURUSAGAMBA**

Kata ya Murusagamba ina umbali wa km 118 kutoka katika makaomakuu ya Wilaya ya Ngara, Mashariki imepakana na Wilaya ya Biharamulo, Magharibi imepakana na Kata ya Muganza, kaskazini imepakana na Kata ya Nyamagoma na kusini imepakana na Mkoa wa kigoma na nhi jirani ya Burundi.

Ina jumla ya vijiji 3 vyenye vitongoji 21, kaya 2470 na jumla ya watu15547 ambapo wanaume ni 6003 na wanawake 9544

Vikao vya kisheria vilivyofanyika Januari mpaka Machi 2106, Kamati ya Maendeleo ya kata (WDC) kikao 1, ulinzi na usalama Kata vikao 3, Serikali ya kijiji vikao 6 vikao 3 havikufanyika, ulinzi na usalama vitongoji vikao 6 vikao 3 havikufanyika, ulinzi na usalama vijijini vilifanyika vikao 6 vikao 3 havikufayika, mikutano mikuu ya vijiji ilifanyika mikutano 2 mmoja haukufanyika.

Uandikishwaji wa wanafunzi wa madarasa ya awali jumla ya wanafunzi walioandikishwa katika shule ya Murusagamba, Ntanga na Murugina jumla walikuwa 985, wanafunzi wa darasa la kwanza jumla walikuwa 312

Wakazi wanaoishi katika Kata ya Murusagamba wanajishughulisha na kilimo, ufugaji, miradi midogo midogo ya kiuchumi, na biashara.

Mapato na matumizi katika Robo ya III, mapato yanayopatikana katika soko la kata Murusagamba 1,808,500/=, Magamba Tshs. 3091,000/= na zilitumika zote, Ntanga Tshs. 5,000,000/= na zilitumika zote, Murusagamba Tshs.671,100/=

Mapato katika sekta ya afya, Kituo cha afya Tshs. 3,935,169/= matumizi yalikuwa Tshs. 1,595,400/= salio lililobaki ni Tshs. 2,339,769/=, Magamba zahanati Tshs. 2,260,868.89/= matumizi Tshs. 740,000/= salio lililobaki ni Tshs. 1,520,868.89/=, Ntanga zahanati Tshs. 7,825,487.89/= hazijatumika.

Fedha za ruzuku shule ya msingi Murugina Tshs. 1,382,000/= matumizi Tshs.656,000/= salio lililobaki ni Tshs. 734,777.41, shule ya msingi Murusagamba Tshs. 917,000/= matumizi Tshs. 542,700/= salio lililobaki ni Tshs. 374,300/= shule ya msingi Ntanga Tshs. 748,000/= matumizi Tshs. 357,000/= salio lililobaki niTshs. Tshs. 391,000/=

Baraza la Kata lipo na linaendelea na kazi zake kwa mujibu wa sheria, changamoto zinazoikabili baraza ni kutokuwa na vitendea, mafunzo na posho.

Hali ya ulinzi na usalama ni shwari.

Changamoto zilizopo katika kata, jengo la upasuaji haliendelei, upungufu wa wataalam wa

ugani, uhaba wa mafuta ya petrol na vipuli vya pikipiki, kutopatiwa vitendea kazi vya ofisi ya kata na vijiji, machinji yameharibika, uhaba wa nishati na umeme, uhaba wa maji, jengo la zahanati Ntanga ni bovu n.k.

**KATA YA NTOBEYE**

Vikao vya kisheria vilivyofanyika katika Kata ya Ntobeye WDC vilifanyika vikao 3 viwili vilikuwa vya dharura, vikao vya VDC kijiji cha Chivu 2, Ntobeye 3, Runzenze 3, Kigina 3, Vikao ngazi ya Kitongoji, Chivu 5, Ntobeye 9, Runzenze 5 na kigina 4, Mikutano mikuu iliyofanyika jumla ilikuwa 4

Mapato na matumizi katika Kata ya Ntobeye, wananchi walichangia ujenzi wa miundombinu kwenye maabara ya Sekondari ya Ntobeye ambapo shughuli iliyofanyika ni ujenzi wa meza kwa kutumia matofari na zege na utengenezaji wa stuli 20, jumla ya michango iliyopatikana ilikuwa ni Tshs. 2,025,500/=

Vyanzo vingine vya mapato, kijiji cha Chivu mapato Tshs. 170,000/= matumizi Tshs.151,700/= baki Tshs. 18,300/=, Ntobeye mapato 306,700/= matumizi Tshs. 125,000/= baki Tshs.181,300/=, Runzenze mapato 220,000/= matumizi 182,000/= baki Tshs. 38,000/= kigina hakuna.

Fedha za ruzuku mashuleni mapato katika shule zote 4 yaani Ntobeye, Chivu, Nyakariba, Murukagati na kigina jumla iliyoletwa ilikuwa Tshs. 5,757,000/= jumla ya matumizi kwa shule zote ni Tshs.3,114,000/= salio lililobaki 2,643,000/=

Wagonjwa waliopelekwa katika zahanati ya Ntobeye kuanzia mwezi Januari mpaka Machi jumla walikuwa 1,766, Tshs. 1,356,000 zilipelekwa kama michango ya CHF, UF na NHIF.

Shughuli za kiuchumi katika Kata ya Ntobeye ni kilimo na ufugaji

Kata ya Ntobeyeilibahatika kuwa miongoni mwa kata zilizowekwa kwenye mpango wa TASAF III, vijiji 3 vilihusishwa na mpango huu, vijiji hivyo ni Runzenze, Kigina na Ntobeye. Katika kijiji cha Ntobeye TASAF III ina mpango wa kuanzisha mradi wa uchimbaji wa visima 7 vyenye mita na ujazo 72 pia mradi wa upandaji wa vitalu vya miti katika eneo kubwa lenye hekta 19.7

Miradi ya Maendeleo katika Kata ya Ntobeye, kununua seti za vifaa vya chanjo, kununua vitendanishi vya maabara, kuanza ukarabati wa mradi wa maji chivu A na B, kuhamasisha uzalishaji wa mnazao ya kilimo ya aina zote, kuanzisha shamba moja la mfano la kahawa, ujenzi wa matundu ya vyoo 5 katika shule ya msingi Chivu na 5 katika shule ya msingi Murukagati, ujenzi wa bweni 1 shule ya sekondari Ntobeye, kufanya matengenezo ya kawaida barabara ya Chivu-Ntobeye-Nyakiziba, kufanya matengenezo ya kawaida katika barabara ya Murugwanza-Runzenze, kufanya matengenezo ya sehemu korofi katika barabara ya Mukididili-Chivu-Kigina shule ya msingi km 8

Changamoto zilizoko katika Kata ya Ntobeye, upungufu wa miundo mbinu kama nyumba za waalimu, madarasa, madawati na matundu ya vyoo, upungufu wa waalimu wa masomo ya hisabati na sayansi, mwitikio mdogo wa wananchi kujiunga na mfuko wa afya ya jamii

(CHF), Kutoletwa kwa fedha za miradi ya maendeleo.

Ujenzi wa maabara unaendelea vizuri vyumba 3 vimeshakamilika hadi hatua ya majengo. Katika kipindi cha Januari mpaka Machi kazi iliyofanyika ni ujenzi wa meza kwa kutumia matofali na zege wanasubiri masinki toka Halmashauri na utengenezaji wa stuli 20.

**KATA YA KIBIMBA**
Kata ya Kibimba ina vijiji 4 na vitongoji 20, kuna kaya 2732 zenye wakazi15071 ambapo wanaume 6861 na wanawake 7710

Kata ya kijamii ina shule za msingi 5 na shule ya sekondari 1, chuo cha ufundi cha ushirikala REDESO chini ya usimamizi wa VETA, zahanati 4, 3 ni za serikali na moja inamilikiwa na kanisa katoliki la Rulenge-Ngara, uwanja wa ndege wa kimataifa Ruganzo uliopata umaarufu kipindi cha wakimbizi wa Rwanda na Burundi mwaka 1993-2011

Shughuli za kiuchumi katika kata ya Kibimba ni pamoja na kilimo cha chakula, mbogamboga, na mazao ya biashara, ufugaji wa wanyama kwa ajili ya mbolea, maziwa na nyama.

Hali ya ulinzi na usalama ni shwari hakuna matukio ya kutishia amani wananchi.

Vikao vya kisheria WDC kilifanyika kikao 1, Halmashauri ya kijiji vilifanyika vikao 12, Mikutano ya vitongoji ilifanyika 32, mikutano 28 haikufanyika, mikutano ya kijiji ilifanyika 3 mmoja haukufanyika.

Mapato na matumizi ya Kata ya Kibimba, mapato ya vijiji, kijiji cha Buhororo mapato ni Tshs. 9,055,776.76/= matumizi Tshs. 9,055,776.76/=, Kumtana mapato ni Tshs. 5,601,886.36/= na matumizi ni Tshs. 5,601,886.36/=Ruganzo mapato Tshs. 323,250/= matumizi ni Tshs. 93,250/= salio lililobaki ni Tshs. 230,000/=.

Mapato katika shule za msingi jumla ilikuwa ni Tshs. 4,908,099.00/= matumizi ni Tshs.2,349.200/= salio lililobaki ni Tshs.2,558,899.95, shule ya sekondari Kibimba mapato ni Tshs. 1,180,000/= matumizi ni Tshs. 250,000/= salio lililobaki ni Tshs. 930,000/=.

Zahanati ya Rugazo mapato Tshs. 274,000/= matumizi ni Tshs. 259,500/= salio lililobaki ni Tshs. 15,500/=, zahanati ya Kumtana mapato ni Tshs. 1,080,000/= matumizi ni Tshs. 724,000/= salio lililobaki ni Tshs. 356,000/=, zahanati ya Mayenzi mapato ni Tshs. 1, 547,415/= matumizi ni Tshs. 814,000/= Salio lililobaki ni Tshs. 733,415/= Tshs. 239,200/= zilikusanywa na kuwasilishwa Halmashauri
Miradi ya maendeleo katika Kata ya Kibimba, ujenzi wa nyumba ya Mganga vifaa vimekamilika wanasubiri nguvu ya serikali, ukamilishwaji wa nyumba ya waalimu 2 vifaa vimekamilika wanasubiri nguvu toka serikalini, ujenzi wa ofisi ya kijiji jengo limekamilika bado kukabidhiwa, pembejeo za kilimo kwa walengwa 150 wakulima 80 walishapokea bado wakulima 70, ujenzi wa maktaba ya shule ya msingi Buhororo ujenzi umekamilika na kukabidhiwa, ujenzi wa shule ya msingi Ruganzo shule imefikia darasa la 4 kuna madarasa 2 na moja la juda ambalo limejengwa la muda, ujenzi wa maabara 2 katika shule ya sekondari vyumba 2 vimekamilika bado chumba 1 kuweka visahani

Changamoto zilizoko katika Kata ya Kibimba, ukosefu wa fedha kukamilisha miradi, kutofanyika kwa vikao kutokana na uelewa mdogo wa Wenyeviti wa Vitongoji, ubebaji wa mimba mashuleni hasa shule za sekondari mpaka sasa wanaume 2 wamefikishwa mahakamani.

**KATA YA MABAWE**

Kata ina vijiji 5 Murugina, Mkaliza, Kumwuzuza, Murugarama na Muhweza, ina vitongoji 22. Ina wakazi 124440 kati ya hao wanaume ni 5915 na wanawake 6525.

Utekelezaji wa shughuli za maendeleo katani unazingatia sekta zote yaani elimu, Afya Maji, kilimo mifugo na ushirika, utawala, maendeleo ya jamii, maliasili na mazingira, ardhi na suala zima la ulinzi na usalama katika kata linaendelea kuimarishwa.

Vikao vya kisheria, Kamati ya maendeleo ya Kata 1, ulinzi na usalama ya Kata 3.

Ngazi ya vijiji Murugina Halmashauri kuu ya kijiji 3, mikutano mikuu 1, kamati ya ulinzi na usalama 3, Mukaliza Halmashauri ya kuu ya kijiji 3, mikutano miku 1 na kamati ya ulinzi na usalama ya kijiji 3, Kumwuzuza Halmashauri kuu ya kijiji 3, mikutano mikuu 1, kamati ya ulinzi na usalama ya kijiji 3, Murugarama Halmashauri ya kuu ya kijiji 3, mikutano mikuu 1, Muhweza Halmashauri kuu ya kijiji 3, mikutano mikuu 1, kamati ya ulinzi na usalama 3.

Ngazi ya kitongoji mikutano mikuu iliyofanyika 25 ambayo haijafanyika 45, kamati ya ulinzi na usalama mikutano iliyofanyika 57 ambayo haijafanyika 9

Shughuli za baraza la kata zinaendelea kuna changamoto ya ukosefu wa vitendea kazi

Utekelezaji wa miradi ya maendelo, maandalizi ya ujenzi wa vymba 2 vya madarasa na ofisi ya M/Mkuu wa shule ya msingi Mukibengere katika kijiji cha Murugina eneo la ujenzi kuna matofali 15,000 na usombaji wa vifaa unaendelea, ujenzi wa maabara 3 kwa kujenga chumba 1 kipya na kubadilisha vymba 2 vya madarasa katika shule ya sekondari Mabawe ujenzi wa vymba vyote 3 umekamilika bado samani na mfumo wa umeme, ujenzi wa kituo cha kuchakata kahawa katika kijiji cha Murugina ujenzi upo katika hatua ya kufunga mashine na mfumo wa maji, ujenzi wa nyumba ya kusimika mashine ya kusindika muhogo kijiji cha Murugina ujenzi wa nyumba umekamilika na ufungaji wa mashine uko katika hatua ya mwisho

Hali ya ulinzi na usalama ni nzuri na kuna suala la ujambazi na kutumia silaha za moto uliojitokeza katika Robo ya III mnamo tarehe 8/2/2016, hali ya ulinzi shirikishi ni nzuri

Mapato yaliyokusanywa, ushuru wa masoko Tshs. 1,333,000/=, ushuru wa mazao Tshs. 1,397,800/= jumla kuu ni Tshs. 2,730,000/=

Changamoto zilizoko katika kata, wananchi kutochangia kwa hiari kwa ajili ya maendeleo, kukosekana kwa vitendea kazi, ukosefu wa fedha za ruzuku toka serikalini, jamii kutoshiriki katika mikutano mbalimbali, upungufu wa madawa katika kituo cha afya

Mabawe.

Kata ya Mabawe ina shule ya sekondari 1 ambayo ina wanafunzi 368 wavulana 167 na wasichana 201

**KATA YA NYAKISASA**

Kata ya Nyakisasa ni miongoni mwa Kata 9 zinazounda Tarafa ya Rulenge, inaundwa na vijiji 4, vitongoji 19. Ina jumla ya kaya 5167 na idadi ya wakazi 23434, wanaume 11365 na wanawake 12069. Watumishi walioko kwenye Kata ya Nyakisasa Mtendaji wa Kata 1, MEK 1, Mkuu wa s/s 1, Afisa kilimo 1, Afisa mifugo 1, Afisa afya1, O/A wa Kata 1, Watendaji wa kijiji 3 na mmoja kijiji cha Kashinga wa muda hana ajira ya kudumu.

Taasisi zilizoko katani, shule ya sekondari 1, zahanati 3, Mahakama ya mwanzo 1(haifanyi kazi), Madhehebu ya dini 6 (wakristo na waislam), amani zilizoko katika ofisi ya kata benchi 6, meza 5.

Mikutano ya kijiji ngazi ya WDC vilifanyika vikao 3 kimoja hakikufanyika, ulinzi na usalama vilifanyika Kashinga 7, Kumugamba 6, Nyamahwa 6 na kigoyi 5, viwili havikufanyika, mikutano ya kijiji iliyofanyika ni 3 mmoja haukufanyika, mikutano mikuu iliyofanyika 3 na mmoja haukufanyika

Miradi ya maendeleo iliyoko kayika kata ya Nyakisasa, ujenzi wa nyumba za waalimu imefikia hatua ya linta, ujenzi wa vymba 2 vya madarasa shule ya sekondari Nyakisasa vyumba vimeezekwa, ujenzi wa vyoo vya watumishi na wanafunzi shule ya sekondari matundu 10 vimefikia ujenzi wa boma.

Idadi ya waalimu wa shule za msingi na sekondari, shule za msingi wanaume ni 68, na wanawake 25 jumla wapo 93, shule za sekondari wanaume 12 wanawake 3 jumla wapo 15. Idadi ya wanafunzi wa shule za awali, I-IV wanaume 2295 na wanawake 2198 jumla wapo wanafunzi 4493. Wanafunzi wa MEMKWA katika kituo cha Mikole wapo 37, wanaume 20 na wanawake 17, kituo cha Ntukamazina wapo 75, wanaume 40 na wanawake 35.

Mapato ya shule za msingi Kata ya Nyakisasa jumla ya fedha zilizoko benki ni Tshs. 6,644,409.88 zilizotumika ni Tshs. 3,078,000/= salio lilibaki benki 3,566,409.88/=

Miundo mbinu iliyoko kwenye kata, kuna josho, kibanio na maeneo ya malisho na mashamba kwa ajili ya wafugaji na wakulima.

Changamoto zilizopo kwenye Kata, uchache wa vibanio, barabara chakavu, watumishi wa Kata hawana usafiri, mafuta kwa ajili ya kuzungukia miradi na shajara za ofisi.

**KATA YA BUGARAMA**

Kata inaundwa na vijiji 3 na vitongoji 13, ina jumla ya kaya 3348 zenye wakazi 14214, kijografia inapakana na Kata ya Kibogora kwa upande wa magharibi, upande wa mashariki inapakana na Kata ya Muganza na upande wa kaskazini inapakana na Kata ya Bukiriro na upande wa kusini nchi ya Burundi.

Hali ya ulinzi na usalama ni nzuri, kuna kituo kidogo cha polisi na kituo kidogo cha jeshi la wananchi la Tanzania

Vikao vya kisheria, mikutano mikuu ilifanyika kwa 100%, Kamati za Halmashauri za vijiji vimefanyika 9, kamati za maendeleo ya kata (WDC) kimefanyika 1

Kata ina Baraza la Kata ambalo lina wajumbe 8 kutoka katika kata ya Bugarama na Kibogora

Miradi ya Maendeleo, kuna ujenzi wa vyoo matundu 6 shule ya msingi Rwinyana michango ya wananchi inaendelea, ukarabati wa milango na madirisha ya vyumba vya madarasa shule ya msingi Bugarama fedha Tshs. 504,000/= kutoka elimu msingi bure, ujenzi wa vyoo matundu 2 zahanati ya Mumiramira wananchi wamechanga Tshs. 750,000/= na kabanga nickel wamechangia vifaa vya kiwandani.

Vyanzo vya mapato ni magurio 3 na fedha iliyokusanywa ni nTshs. 1,159,000/=

Fedha za ruzuku za elimu bure katika shule za msingi 4 fedha iliyopokelewa ni Tshs. 3,154,000/= na zilizotumika ni Tshs. 2,120,000/=, michango ya CHF fedha iliyokusanywa ni Tshs. 470,000/=
Changamoto zilizopo katani, ukosefu wa vifaa vya ofisi ya vitongoji, vijiji na kata, vitendea kazi, mafunzo kwa wajumbe wa Baraza la Kata hayakutolewa, upungufu wa nyumba za waalimu, upungufu wa madarasa, upungufu wa samani, upungufu wa watumishi wa afya, ukosefu wa madawa na vifaa tiba, ukosefu wa zahanati kijiji cha Rwinyana.

**KATA YA KANAZI**
Kata ya Kanazi iko umbali wa km 9 kutoka katika makao makuu ya Wilaya ya Ngara upande wa magharibi, ina jumla ya vijiji 6 vitongoji 24, ina jumla ya kaya 3748, kati yao wanawake ni 9389 na wanaume. Wakazi wa Kata ya Kanazi wanajishughulisha na kilimo cha mazao ya chakula, na biashara. Kulikuwa na changamoto mbalimbali katika zoezi la pembejeo kama vile kuletwa nje ya msimu, gharama za pembejeo kuwa kubwa, imani potovu walizonazo wakulima kuhusu utumiaji wa pembejeo kamati ya pembejeo ya kijiji kukosa motisha ya usafiri ili kuzungukia walengwa na kutoa elimu juu ya faida ya kutumia pembejeo.

Kata ina jumla ya vikundi vya kiuchumi 51 ambavyo vinafanya shughuli mbalimbali kama vile kilimo cha mbogamboga, biashara ndogo ndogo, ufugaji wa mbuzi na kuku na kilimo cha migomba, kilimo cha kahawa, Bustani ya miti, Vicoba, salon, daladala, maduka ya rejareja uselemala na n.k

Kata ina viongozi wa kuchaguliwa kama vile wenyeviti wa vitongoji 24, wenyeviti wa vijiji 6, wajumbe wa serikali ya kijiji 150, pia kuna watendaji wa serikali/kata/kijiji kama vile watendaji wa kijiji 4 na wanaohitajika ni 6

Vikao vya kisheria vilivyofanyika Kamati ya maendeleo ya Kata (WDC) vilifanyika vikao3, kamati ya ulinzi na usalama Kata vilifanyika vikao 9, Serikali ya Kijiji vikao 44 ambavyo

havikufanyika ni 10, Kamati ya ulinzi na usalama ya kijiji vikao vilivyofanyika ni 47, Mikutano mikuu ya vijiji ilifanyika vikao 13, Mikutano mikuu ya vitongoji vilivyofanyika jumla vilikuwa ni 109

Changamoto zilizokuwepo ni pamoja na kutokuapisha kwa wajumbe wa VDC, VEO's kuwa na ajira za muda hivyo kusababisha kutofanyika kwa vikao vya kisheria., Wenyeviti wa vitongoji kutokuwa na vitendea kazi

Mapato na matumizi katika kata ya Kanazi, soko la Kanazi januari mpaka Februari 2016 walikusanya jumla ya Tshs. 7,052,000/=, michango ya maendeleo ya miradi katika vijiji kwa kipindi cha julai 2015 mpaka machi 2016 jumla zilikusanywa kiasi cha Tshs. 1,574,500, zilitumika 1,435,725/= na salio lililobaki ni Tshs. 138,775/=, makusanyo ya zahanati kata ya Kanazi kwa michango ya huduma ya papo kwa papo, NHIF na CHF jumla yalikuwa ni Tshs. 4,233,405/=

Miradi ya maendeleo iliyotekelezwa, ujenzi wa choo soko la Kanazi matundu 2 choo imekamilika ila bado haijatumika, ujenzi wa nyumba ya Mganga zahanati ya kabalenzi nyumba imekamilika, ujenzi wa choo shule ya msingi kabalenzi matundu 8 choo imefikia hatua ya kuezeka, ujenzi wa choo matundu 8 shule ya msingi Nyarusange kanazi choo imefikia hatua ya kufunika shimo kwa zege inasubiri kupandisha boma

Mapokezi ya fedha za ruzuku kwa kila shule Julai mpaka Machi jumla zilipokelewa Tshs. 7,673,814.77 jumla zilitumika Tshs. 5,273,440.00/= na salio lililobaki lilikuwa ni Tshs. 2,400,374,00/=

Uandikishwaji wa wanafunzi wa awali, wavulana walikuwa 599 na wasichana 576 jumla 1175, walioandikishwa darasa la kwanza kwa shule zote wavulana 374 na wasichana 333 jumla walikuwa 707
Changamoto zilizoko katika kata ya Kanazi, utoro wa wanafunzi, upungufu wa waalimu wa masomo ya sayansi na hisabati, tatizo la umeme na maji.

Maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi katika kata ya Kanazi, walijikubali jumla wapo 34 wanaume 14 na wanawake 20, wapo ambao tayari wameshajisajili na wnakikundi cha kilimo cha mihogo na shamba la migomba, hali zao zinaendelea kuwa nzuri. Kamati za ukimwi kwa vijiji vyote zipo.

Malipo ya ruzuku ya kunusuru kaya maskini TASAF III, mradi upo katika vijiji vya Mukarehe, Mukibogoye na Kabalenzi na jumla ya Tshs. 19,738,818.19/= zilitolewa kwa walengwa.

**KATA YA KIBOGORA**
Kata ya Kibogora ipo km 80 toka katika makao makuu ya Wilaya ya Ngara, ina vijiji 2 kihinga na Nyarulama ina jumla ya kaya 3434, wakazi 14870 ambapo wanaume ni 6435 na wanawake ni 8435. Aidha Kata ya kibogora ina jumla ya vitongoji 9

Vikao vya kisheria ngazi ya kitongoji hadi ngazi ya Kata vinafanyika na muhtasari imeshawasilishwa ngazi ya Wilaya.

Michango ya wananchi kuchangia ujenzi wa maabara, Kihinga walichangia Tshs. 600,000/= na Nyarulama walichangia Tshs. 628,000/= bado wananchi wanaendelea kuchangia

Mapato na matumizi yaliyotokana na ushuru wa mazao na ushuru wa soko, ushuru wa mazao Tshs. 257,500/= ushuru wa soko Tshs. 150.000/= jumla kuu Tshs. 407,500/=. Makusanyo ya fedha yaliyowasilishwa Halmashauri, S/M Nyarulama Tshs. 776,000/=, S/M Kihinga Tshs. 862,000/=, S/M Nyarukubala Tshs. 504,000/= na S/Sekondari Kibogora Tshs.986,000/=

Wanafunzi walioandikishwa darasa la awali katika shule ya msingi Kihinga, Nyarukubara na Nyarulama wavulana 581 wasichana 537 jumla 1318, darasa la kwanza wavulana 250 wasichana 225 jumla 475

Mapato yanayotokana na CHF Tshs. 470,000/= malipo ya papo kwa papo Tshs 130,000/=

Hakuna miradi ya maendeleo ndani ya kata ya Kibogora isipokuwa ujenzi wa maabara katika shule ya sekondari ya Kibogora kwa kushirikiana na Kata mama ya Bugarama.

Hali ya ulinzi na usalama ni shwari na wananchi wanendelea kufanya shughuli zao bila kubuguziwa, kituo kidogo cha polisi na jeshi la wananchi kituo cha Bugarama wanafanya kazi yao ipasavyo.

**KATA YA MUGOMA**

Kata ya Mugoma ina wakazi 15068, ambapo wanaume 7402 na wanawake 7666, wapo viongozi wa kuchaguliwa, watumishi na wafanyakazi wa umma

Kata ya Mugoma inalipongeza shirika la TUMAINI FUND kwa kuratibu shughuli za ukimwi chini ya hospitali yaMurugwanza kwa sababu wanatoa dawa za ukimwi na matumizi ya Condom

Hali ya kiuchumi, wakazi wanajishughulisha na shughuli za kilimo, ufugaji na biashara.

Vikao vya kisheria, WDC kilifanyika kikao 1, VDC vimefanyika 15, mikutano mikuu ya vijiji 15 na mikutano ya vitongoji ilifanyika 57 ambayo haijafanyika ni 9

Mapato na matumizi, ushuru wa beria Tshs. 272,500,ushuru wa soko Tshs.100,000/=, ushuru wa mbao 100,000/=, ushuru wa machinjio Tshs. 39,000/=.

Utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ujenzi wa maabara shule ya sekondari Mugoma na Muuvyagira ukamilikaji wa majengo unaendelea, ujenzi wa kituo kipya ujenzi uko usawa wa linter, ujenzi wa nyumba ya mwalimu Muruvyagira sekondari ujenzi bado kuanza, ukamilishaji wa nyumba bora ya mfano kijiji cha Mukikomero boma imeezekwa na kukamilika, kupewa pembejeo za kilimo kijiji cha Muruvyagira, kununua na kusambaza mashine za kukoboa kahawa ya kijiji cha Shanga na Mugoma fedha hazijatolewa, kuanzishwa kwa shamba darasa la kahawa kwa vijiji vya Shanga na Mugoma mradi bado

kuanza, ujenzi wakituo cha kuchakata kahawa na mfumo wa maji Mugoma uko katika katua za mwisho kukamilika

Fedha za ruzuku kwa shule za msingi Mugoma Tshs. 891,410.43/= na zilizotumika Tshs. 400,334/=, shule ya msingi Shanga Tshs. 1,253,380.10/= na matumizi Tshs. 841,900/=, shule ya msingi Mubuhenge Tshs. 1,478,660.80/= matumizi 923,260.80/=, shule ya msingi Mukagugo Tshs. 959,883.23/= matumizi Tshs.882,000/= shule ya msingi Mugikomero Tshs. 376,234.08/= matumizi Tshs. 217,500/= Shule ya sekondari Mugoma mapato ni Tshs. 2,814,000/= matumizi 2,357,900/= Shule ya sekondari Muruvyagira Tshs. 1,294,000/= matumizi Tshs. 205,000/=

Changamoto zilizoko katani , ukosefu wa zahanati, wakandarasi kutokamilisha miradi, ukosefu wa ofisi ya serikaliya kijiji Muruvyagira

**KATA YA NGARA MJINI**
Mamlaka ya Mji mdogo wa Ngara ndio mji mdogo wa kwanza kuanzishwa hapa Wilayani kwa kufuata na kuzingatia sheria za uanzishwaji wa Mamlaka za mji midogo hapa nchini.

Mamlaka ya mji mdogo inaundwa na vitongoji 17 vinavyotokana na vijiji 4 kabla ya kufutwa. Mamlaka ya mji mdogo iko makao makuu ya Wilaya, upande wa mashariki inapakana na Kata ya Nyamiaga, Upande wa kusini inapaka na Kata ya Kibimba, upande wa Kaskazini inapakana na kata ya Ntobeye, upande wa Magharibi inapakana vile vile na Kata ya Kibimba na upande wa Kaskazini Magharibi inapakana na Kata ya Kanazi kijiji cha Mukirehe. Kuna ofisi mbalimbali za Serikali kuu na Serikali za Mitaa na Idara zake mbalimbali zenye watumishi wa kada mbalimbali. Ina kaya 4,366 wakazi 20,968 wanawake 11,164 na wanaume ni 9,804.

Wakazi wanajishughulisha na kilimo, biashara, ufugaji na baadhi ya watumishi wa Serikali na taasisi zisizo za Serikali. Vyanzo vya mapato katika eneo la Mamlaka ya Mji mdogo hutegemea ushuru wa masoko hasa masoko ya kojifa, Mukididili, Murugwanza na Ngara mjini pamoja na soko la ndizi karibu na benki ya CRDB.

Fedha za elimu bure zilizoletwa katika shule za msingi kuanzia mwezi Januari mpaka Machi zilikuwa kama ifuatavyo; Ngara mjini Tshs. 1,274,000/=, Murugwanza Tshs. 960,600/=, Ngara mjini elimu maalum Tshs. 2,675,000/= Murugwanza elimu maalum Tshs. 2,675,000/=, Nakatunga Tshs. 737,000/=, Nyamiaga Tshs. 1,071,000/=, Mukididili Tshs. 781,000/=, Mubinyange Tshs. 306,600/= Jumla kuu Tshs. 10,480,200/=

Mamlaka ya Mji mdogo ina sekondari 2 za Serikali ambazo ni Murugwanza na Ngara sekondari. Kuna hospitali 2 ya Nyamiaga ambayo ni ya Serikali na Hospitali ya Muruganzwa ambayo inamilikiwa na Kanisa la Anglikani Dayosisi ya Kagera. Lipo Baraza moja ambalo hukutana mara moja kwa wiki yaani Jumanne ili kutatua migogoro mbalimbali ya ardhi japo lina changamotombalimbali na hasa vitendea kazi na upatikanaji wa fedha za uendeshaji.

Vikao vya kisheria vilivyokwisha kufanyika ni 2 vya mipango na fedha, utawala na mipango miji na vingine vilishindikana kwa sababu ya ukosefu wa fedha za uendeshaji wa

vikao hivyo na shughuli mbalimbali.

Suala la ulinzi na usalama liko vizuri maana hakuna mambo hatari yanayosababisha kutokuwepo na amani na usalama ingawa vikao havijakaa kwa sababu ya changamoto mbalimbali.

Miradi inayotekelezwa, kuna ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa, matundu 10 ya vyoo 8 kwa ajili ya wanafunzi na 2 kwa ajili ya waalimu katika shule ya sekondari Murugwanza ambapo msingi wa vyumba vya madarasa umekamilika na matundu ya vyoo (septic tank) yamekamilika, ujenzi wa barabara kilometa 3 za muda maalumu zinaendelea katika hatua nzuri, ujenzi wa kituo cha kupimia watoto na akina mama wajazitokatika kitongoji cha Nakatunga, uboreshaji wa vyanzo vya maji vya asili vilivyoko Nyakabonde, Kabonde, Mkigorogoro, Mukavugo na Gwamiheha, upimaji wa viwanja kwa maeneo yote Mamlaka ya mji mdogo, upatikanaji wa umeme kwa bei nafuu kutokana na kipato cha wakazi wengi kuwa na kipato cha chini (umeme wa REA) katika vitongoji vyote, ujenzi wa dampo la kutupa taka.

Changamoto zilizoko katika shule za sekondari ni upungufu wa madawati na meza, matundu ya vyoo, maji kutopatikana (miundo mbinu ya maji), upungufu wa waalimu wa sayansi.

Wanafunzi walioandikishwa shule, shule ya msingi Mubinyange waliandikishwa watoto 110, wavulana 54 na wasichana 56, darasa la awali wanafunzi 113, wavulana 59 na wasichana 54. Shule ya msingi Nyamiaga darasa la 1 wanafunzi 87,wavulana 42 na wasichana 45, darasa la awali wanafunzi 62, wavulana 34 na wasichana 28. Shule ya msingi Murugwanza darasa la 1 waliandikishwa wanafunzi 144, wavulana 76 na wsichana 68, darasa la wanafunzi awali 147, wavulana 80 na wasichana 67. Shule ya msingi Mukididili darasa la 1 waliandikishwa wanafunzi 107, wavulana 48 na wasichana 59, darasa la awali wanafunzi 150, wavulana 69 na wasichana 81. Shule ya msingi Nakatunga darasa la kwanza waliandikishwa wanafunzi 174, wavulana 91 na wasichana 83. Shule ya msingi Ngara mjini waliandikishwa wanafunzi 275, wavulana 137 na wasichana 138, darasa la awali wanafunzi 149, wavulana 77 na wasichana 72.

Changamoto ya kiutawala iliyokuwepo, baadhi ya viongozi wa Mamlaka ya mji mdogo hawakubaliani na uwepo wa Mtendaji wa Kata, hivyo ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji na Mwanasheria ijitahidi kutatua tatizo na kutoa ufafanuzi wa kisheria kuhusu uwepo wa Mtendaji wa Kata katika Mamlaka ya Mji mdogo Ngara.

**KATA YA MURUKULAZO**

Kata ya Murukulazo inapakana na kata 3 na nchi ya jirani ya Rwanda, upande wa kusini inapakana na Kata ya Nyamiaga, upande wa kaskazini inapakana na Kata ya Rusumo, upande wa mashariki inaendelea kupakana na Kata ya Rusumo, upande wa magharibi inapakana na kata ya Ntobeye na upande wa kaskazini maghraibi inapakana na nchi jirani ya Rwanda. Kata inaundwa na vijiji 5 ambavyo ni Murukulazo, Kyenda, Burengo, Kagari na Nyakiziba, Kata inaundwa na vitongoji 26 viongozi wa kuchaguliwa 121, vikao vya kisheria vinafanyika ila kuna changamoto vikao kutofanyika kwa wakati na muhtasari haiwasilishwi kwa wakati, shughuli za Baraza zinaenda vizuri kuna changamoto ya

kushindwa kutatua mabo machache kupelekea kuyapeleka mahakamani kwa ajili ya ufumbuzi zaidi.

Vyanzo vya mapato katika Kata ya Murukulazo ni pamoja na soko la Murunyinya na ushuru wa nyama, kuna vyanzo vingine ambavyo haviko hai kama vile mnara wa simu, mchanga na mawe.

Miradi ya maendeleo iliyotekelezwa kuanzia Januari mpaka Machi, ujenzi wa meza 33 za maabara za phyzikia na kemia zimetengenezwa flemu 11 za chumba kimoja cha phyzikia vingine bado ujenzi unaendelea kwa ngazi ya Halmashauri imeleta vifaa vya ujenzi kama saruji mifuko 75, wayameshi 30, vigae na misumali kilo 5, ujenzi wa matundu ya 12 shule ya msingi Burengo vifaa vipo mashimo yameshachimbwa, usambazaji wa pembejeo za ruzuku kwa wakulima usambazaji unaendelea kwa baadhi ya wakulima walipokea mifuko 10 tu, kilimo cha mihogo kinaendelea shamba darasa,ukarabati wa vyanzo vya maji wananchi wamechangia Tshs.1,500,000/ kwa ajili ya kuanza ujenzi, mradi wa kunusuru kaya maskini TASAF III katika kijiji cha Nyakiziba jumla ya kaya 313 zinaendelea kupokea ruzuku kutoka katika mradi huu.

Hali ya ulinzi na usalama ni shwari.

**KATA YA RULENGE**

Kata ya Rulenge inapatikana kusini mwa Wilaya ya Ngara ni miongoni mwa Kata 2 zilizoko katika Mamlaka ya Miji midogo katika Wilaya ya Ngara. Mamlaka ya mji Mdogo Rulenge imeundwa na mitaa 17, kati ya mitaa hiyo mitaa 2 inaongozwa na Wenyeviti wa chama cha CHADEMA, na Wenyeviti 15 ni wa Chama cha Mapinduzi.

Mamlaka ya Mji mdogo Rulenge una jumla ya kaya 3,950 wanaume 8,252 na wanawake 9,061

Shughuli za maendeleo zinazingatia sekta zote yaani kilimoelimu, uvuvi na ushirika, ulinzi na usalama pamoja na ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri

Mji mdogo Rulenge una viongozi mbalimbali, Afisa Mtendaji wa Kata, TEO, Kaimu Afisa Tarafa, Afisa Maendeleo ya Jamii, Afisa Afya,Mtaribu Elimu Kata, Afisa Kilimo, Afisa Mifugo, Mhudumu wa Ofisi, pamoja na Diwani wa Kata. Hakuna mlinzi baada ya mlinzi aliyekuwepo kufariki.

Idadi ya wanafunzi wa shule za msingi, wavulana 1827 na wasichana 1835 julma 3662, Idadi ya wanafunzi shule za Sekondari, wavulana 203 na wasichana 281 jumla 484

Miradi ya maendeleo iliyotekelezwa, ujenzi wa choo matundu 6 shule ya msingi Rulenge umekamilika, ujenzi wa matundu 8 ya vyoo shule ya msingi Munjebwe mradi unaendelea

Taarifa yam nada na machinjio ya mbuzi Januari mpaka Machi mapato yaliyopatikana yalikuwa ni Tshs. 1,145,500/=, mapato ya soko, vibanda na mazao jumla yalikuwa 3,734,000/=

**KATA YA KEZA**
Kata ya keza inaundwa na vijiji 2 ambavyo ni Keza na Kazingati, ina vitongoji 9, Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa Vitongoji wapo wote na hakuna nafasi iliyoachwa wazi. Idadi ya wakazi katika Kata ya Keza ni 8944, kaya 2162, wanaume ni 4034 na wanawake ni 4910. Shughuli za kiuchumi katika kata ya Keza ni pamoja na Kilimo, ufugaji na biashara ya vioski, na vilabu vya pombe. Taasisi zilizopo Katani ni shule za msingi 4 na shule ya sekondari 1 na vituo vya chekechea 3, zipo Taasisi binafsi kama vile madhehebu ya dini ya kikristo na kiislam na vikundi 26 vya wajasiliamali.

Vikao vya Halmashauri ya Vijiji vilivyofanyika, Keza vikao 3, Kazingati 2 hakikufanyika kikao kimoja katika kijiji cha Kazingati. Mikutano mikuu iliyofanyika Keza 1, Kangati hawakufanya mkutano. Vikao vya ulinzi na usalama Keza walifanya vikao 2 na kazingazti havikufanyika, Kamati ya maendeleo ya Kata(WDC) keza kilifanyika kikao 1 na 1 hakikufanyika.

Utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Kata ya Keza, ukarabati wa ofisi ya kijiji umekamilika, ujenzi wa tundu la choo ofisi ya kijiji umekamilika, ujenzi wa matundu ya vyoo katika shule ya msingi Rukira umekamilika kwa kutumia nguvu ya wananchi, ujenzi wa matundu 4 ya vyoo ya muda shule ya msingi Keza shughuli ya ujenzi inaendelea kwa njia ya kujitolea. Katika kijiji cha Kazingati ujenzi wa matundu 4 ya vyoo vya muda shule ya msingi Kibiriziya ujenzi umekamilika na yameanza kutumika, ujenzi wa ofisi ya kijiji Kazingati ujenzi umefikia usawa wa boma, ujenzi wa banda la chekechea kituo cha kitovu ujenzi umekamilika, Ujenzi wa banda la chekechea kituo cha Nyanza umekamilika, Ukarabati wa kuezeka vyoo vilivyoezuliwa na upepo shule ya msingi Rwenzaza (matundu 6) ukarabati umekamilika, matengenezo ya barabara ya Nyanza-Rwenzaza shughuli inaendelea.

Miradi ya Kata ipo kama ifuatavyo; ujenzi wa kituo cha polisi umekwama tangu 2012 kwa sababu Mtendaji wa Kata Staford Thomasi kutumia fedha za mradi Tshs.2,400,000/= kwa kuzipeleka katika ujenzi wa maabara yasekondari, Kijiji cha keza ukamilishaji wa maabara ya sekondari kezabado meza,rangi, shutter.

**KATA YA NYAMAGOMA**
Kata ya Nyamagoma inapakana na Wilaya ya Biharamulo, Kakonko na inapakana na Kata ya Keza, Murusagamba na Muganza. Inaundwa na vijiji 3 ambavyo ni Murubanga, Kumubuga na Kititiza, inaundwa na vitongoji 13, ina jumla ya kaya 1343 zenye watu 7,286 kati yao wanaume ni 3425 na wanawake 3861.

Vikao vya kisheria, vikao vya kijiji Murubanga 3, Kumubuga 3, Kititiza 3 na WDC 1, Mikutano ya kijiji Murubanga 1, Kumubuga 1, na Kititiza 1, Mikutano ya Kitongoji Murubanga 21 na Kumubuga 21, ulinzi na usalama Murubanga 3, Kumubuga 3, Kititiza 2, WDC 3.

Wakazi wa kata ya Nyamagoma wanajishughulisha na kilimo, ufugaji na biashara.

Uandikishwaji wa wanafunzi wa darasa la awali katika shule zote 3 za Kahama, Kumubuga

na Kititiza wavulana walioandikishwa jumla walikuwa 219 na wasichana 229, darasa la kwanza wavulana 150 na wasichana 115.

Wanafunzi wanaolipwa na mradi wa kunusuru kaya maskini katika shule ya msingi Kahama wavulana 23 na wasichana 18, Kumubuga wavulana 31 na wasichana 53.

Fedha za TASAF zilizotolewa kunusuru kaya maskini Robo III, kijiji cha Murubanga Tshs. 2,708,000/= na Kumubuga Tshs. 2,916,896.36/= kwa walengwa wa TASAF.

Vyanzo vya mapato ni belia ya Kumubuga.

Changamoto zilizopo katika kata, kuibiwa kwa beria mara kwa mara, kutokuwepo kivuli cha kukaa, magari mengi kupita yakiwa yamelipia ushuru wa mazao toka katika kata mbalimbali, kutokuwepo kwa mawasiliano sababu ya kutokuwepo kwa minara, kutokuwepo kwa baraza la kata, upungufu wa madarasa, kutokuwepo kwa maji safi na salama.

**KATA YA MBUBA**

Kata ya Mbuba inaundwa na vijiji 4 ambavyo ni Mbuba, Kanyinya, Ruhuba na Kumwendo. Ina vitongoji 16 vyenye kaya 2,586 na wakazi wapatao 13,702 wanaume 6775 na wanawake 6927

Hali ya ulinzi na usalama ni shwari kwa kipindi cha mwezi wa kwanza na mwezi wa pili isipokuwa mwezi wa tatu ulijitokeza wizi wa ng'ombe 6 katika kijiji cha Kumwendo mali ya Bw. Dominic Gaspar na baada ya kuwasaka ng'ombe walipatikana katika Kata ya Rulenge sehemu ya Nyanzali na ulinzi umeimarishwa kijiji hadi kijiji.

Huduma za kijamii katika kata ya Mbuba wakazi wanajishughulisha na shughuli za kilimo, ufugaji na biashara ndogo ndogo.

Kuna shule za msingi 4, shule ya msingi Kumwendo, Mbuba, Kanyinya na Ruhuba, shule za sekondari 2, moja ya Serikali inayoitwa Ndomba na ya binafsi 1 ya kanisa katoliki la Rulenge inayoitwa Mtakatifu Joseph, Zahanati 2 za Serikali, Kanyinya na Mbuba. Hali ya kisiasa ni shwari hakuna mgogoro wa vyama na shughuli zinakwenda sawa.

Vikao vya kisheria vilivyofanyika, vikao vya WDC vilifanyika 3, kimoja hakikufanyika, Vikao vya VDC vilifanyika 28 vikao 8 havikufanyika, Mikutano ya kijiji ilifanyika 9 mikutano 3 haikufanyika, Mikutano ya Vitongoji ilifanyika 58 mikutano 110 haikufanyika.

Mapato na matumizi ya vijiji, kijiji cha kanyinya mapato yalikuwa Tshs. 1,305,000/= matumizi Tshs. 1,018,000/= salio ni Tshs. 286,200/=, Kijiji cha Mbuba mapato yalikuwa Tshs. 544,300 matumizi Tshs 290,300/= salio ni Tshs. 254,000, kijiji cha Kumwendo mapato yalikuwa Tshs. 354,000 matumizi yalikuwa ni Tshs. 157,000/= salio lililobaki ni Tshs. 197,000/= Kijiji cha Rujuba hakuna mapato na matumizi yaliyofanyika.
Fedha za capitation katika shule ya sekondari Ndomba jumla ya fedha iliyoletwa ni Tshs. 3,001,825 matumizi ni Tshs. 1,726,550/= na salio lililobaki ni Tshs. 1,275,278/=
Shule za msingi kanyinya fedha iliyoletwa jumla ilikuwa ni Tshs. 1,322,265.68/=

iliyotumika ni Tshs. 9,873,000/= salio lililopo benki ni Tshs. 534,968. 58/=, Shule ya msingi Mbuba fedha iliyoletwa jumla ilikuwa ni Tshs. 1,490,699.92/= iliyotumika ni Tshs. 780,000/= salio lililopo benki ni Tshs. 710,689.92/=, Shule ya msingi Kumwendo fedha iliyoletwa jumla ilikuwa ni Tshs. 1,384, 609.08/= iliyotumika ni Tshs. 871,100/= salio lililopo benki ni Tshs. 513,509.08/= Shule ya msingi Ruhuba fedha iliyoletwa jumla ilikuwa ni Tshs. 6,348,051.28/=, iliyotumika ni Tshs. 2,835,400/= salio lililopo benki ni Tshs. 3,512,651.28/= Mapato ya zahanati ya Mbuba yalikuwa ni Tshs. 651,795/=.

Hali ya maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi, wananchi wana muamko wa kwenda kupima kwenye zahanati isipokuwa hakuna taarifa ni watu wangapi waliokwisha kupima.

Miradi ya maendeleo kwa mwaka 2015-2016, ujenzi wa choo shule ya msingi Ruhuba, shimo limekamilika ujenzi unaendelea, ujenzi wa barabara ya Kumwendo inatengenezwa na wanafunzi wanavuka kwa kutumia mtumbwi kwenda shuleni, mradi wa maji kijiji cha mbuba, mradi umesimama, ujenzi wa meza za maabara shule ya sekondari Ndomba zimeshajengwa bado sinki.

**KATA YA KIRUSHYA**

Kata ya Kirushya ni miongoni mwa Kata 22 zinazounda Halmashauri ya Wilaya ya Ngara na mojawapo ya Kata 5 zinazounda Tarafa ya Kanazi. Kata ya Kirushya ina ina jumla ya wakazi wapatao 12804 kati ya hao wanaume ni 5552 na wanawake ni 7252. Wapo viongozi 27 wa kuchaguliwa ambao ni Diwani 1, Wenyeviti wa vijiji 4, Wenyeviti wa Vitongoji 22, Watumishi walioko masomoni ni 2, Vikao vya kisheria vilivyofanyika kwa ngazi ya Halmashauri ya Kijiji (Mwivuza 3, Murutabo 3, Kasange 3, na Kirushya 3. Mikutano mikuu ya Kijiji iliyofanyika ( Mwivuza 1, Murutabo 1, Kasange 1, Kirushya1), Kamati ya Maendeleo ya Kata(WDC) Kirushya kilifanyika kikao. Changamoto zinazosababisha kutofanyika kwa vikao vya kisheria ni ukosefu wa karatasi. Hakuna mapato na matumizi yaliyopatikana au kutumika kwa kipindi cha mwezi Januari-Machi, 2016. Kwa kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Machi Kata haijakusanya mapato ya Halmashauri kutokana na Kata kutegemea kupata ushuru kutoka kwenye mazao ya msimu. Mapato ya fedha za elimu bure zilizopelekwa katika shule za msingi na Sekondari za Kata ya Kirushya, shule ya msingi MurutaboTshs. 703,000/=, Mwivuza Tshs. 815,000/=, Mwivuza B Tshs.357,000/=, Kasange Tshs.1,091,000/= na Kirushya Tshs. 783,000/=. Jumla ya fedha za elimu bure zilizopokelewa katika shule za msingi ni Tshs. 3,749,000/= Katika shule za Sekondari jumla fedha zilizopokelewa ni Tshs. 3,883,000/=

Hali ya uandikishaji wa wanafunzi kwa darasa la kwanza na awali kwa Kata ya kirushya, kwa darasa la kwanza waliandikishwa wavulana 193 na wasichana 195, jumla ni wanafunzi 388, kwa darasa la awali wanafunzi wa miaka 0-5 wavulana walikuwa 163 na wasichana 176 jumla walikuwa wanafunzi 339, wanafunzi wa miaka 0-6 wavulana walikuwa 131 na wsichana 135 jumla walikuwa wanafunzi 266.

Utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ujenzi wa maabara shule ya Sekondari Kirushya fedha inayotegemewa katika ujenzi ni michango kutoka kwenye kaya zilizomo kwenye Kata na watumishi

Hali ya ulinzi na usalama katika Kata ya Kirushya ni nzuri isipokuwa bado wahamiaji toka

Burundi wanavuka na kuingia katika kijiji cha kasange ambapo ndipo wanapopokelewa na kisha shirika la UNHCR linakuja kuwachukua na kuwapeleka Lumasi.

Matukio yaliyotokea tarehe 4.4.2016 katika kijiji cha Mwivuza, Bw. Kasoni Andrea alijinyonga kwa kutumia kamba ya kufungia mbuzi kutokana na kuumwa kwa muda mrefu.

Maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi katika Kata ya Kirushya yapo japo hakuna takwimu sahihi, pia kuna kikundi cha waathirika na ugonjwa wa ukimwi waliojikubali kinachoitwa umoja group kina jumla ya wanakikundi 28 ambapo wanaume ni 10, na wanawake 18.

**KATA YA KASULO**
Kata hii inaundwa na vijiji 3 ambavyo ni Kasulo, Rwakaremela na Nyakariba ina jumla ya vitongoji 15, Ina jumla ya kaya 3731, idadi ya watu 17032, wanaume 8424 na wanawake 8608, Hali ya ulinzi na usalama ni shwari kidogo kwa wastani kwa maana kwa miezi hiyo kumekuwepo na matukio mbalimbali ya wizi wa pikipiki na hasa mwezi Januari 2016 ikiwa ni pamoja na tukio la mauaji lililotokea 22/01/2016 ya kijana mmoja aliyejulikana kwa jina la joseph Magesa, tarehe 29/01/2016 wananchi wenye hasira wasiojulikana wamechoma na kuvunja nyumba ya Ndg. Tuombe Paschal

Wakazi wa Kabanga wanajishughulisha na kilimo cha mazao ya chakula na biashara, ufugaji na biashara. Makusanyo ya ushuru wa machinjio, stendi, maegesho yaliyofanyika toka mwezi Januari mpaka Machi jumla yalikuwa ni Tshs. 15,695,200/= na makusanyo yam nada wa ng’ombe Lumasi mwezi Januari mpaka Machi ilikusanywa jumla ya Tshs. 23,400,000/=

Michango ya wananchi kwa ajili ya ujenzi wa maabara ya shule ya sekondari Rusumo A jumla ilikusanywa Tshs. 1,519,500/= matumizi yaliyofanyika yalikuwa ni Tshs. 63,500/=

Michango mbalimbali ya wananchi kwa ajili ya shughuli za maendeleo jumla ilikuwa ni Tshs. 1,553,000/= matumizi 802,000/= salio lililobaki ni Tshs. 751,000/=
Fedha zaruzuku zilizopokelewa katika shule za msingi zilikuwa kama ifuatavyo; Kasulo S/M Tshs. 682,000/=, Njiapanda S/M Tshs. 4,294,000/=, Kapfuha S/M Tshs. 315,000/=, Kumnazi S/M Tshs. 1,952,000/=, Kamuli S/M Tshs. 533,000/= Kabaheshi S/M Tshs. 685,000/=, Ngoma S/M Tshs. 8,865,000/=

Fedha zilizopokelewa katika shule ya sekondari za Kasulo; Lukole sekondari Tshs. 49,571,600/= Rusumo A Tshs. 2,297,000/=. Michango ya CHF, NHIF na malipo ya papo kwa papo katika kituo cha afya Lukole jumla zilikusanywa Tshs. 7,766,420/=

Miradi iliyopo katika Kata ya Kasulo, ukamirishaji wa ujenzi wa maabara ya shule ya sekondari Rusumo A, ujenzi wa vibanda vya biashara,.

Usajili wa wananfunzi wa madarasa ya awali wavulana walikuwa 439 na wasichana 418 jumla walikuwa 857, darasa la kwanza wavulana 543 na wasichana 564 jumla walikuwa 1107, kidato cha kwanza wavulana 93 na wasichana 94 jumla walikuwa 187

Changamoto zilizoko Katani ni pamoja wizi wa ng’ombe na pikipiki, upungufu wa

nyumba za waalimu, vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo na madawati katika shule za msingi zilizoko Katani, Mgogoro kati ya kanisa la RC na Serikali ya kijiji cha Rwakalemela, kutopatiwa ufumbuzi wa ukamilishwaji wa masjara ya ardhi ya kijiji.

**KATA YA KABANGA**

Kata ya Kabanga iko umbali wa km 26 kutoka katika makao makuu ya Wilaya ya Ngara, inapakana na Kata ya Mabawekwa upande wa kaskazini na upande wa mashariki inapakana na kata ya Mbuba, upande wa magharibi inapakana nan chi jirani ya Burundi.

Kata ya Kabanga ni miongoni mwa Kata 5 zinazounda Tarafa ya Kanazi na pia ni kati ya Kata 22 zinazounda Halmashauri ya Wilaya ya Ngara, ina jumla ya kaya 4366 zenye jumla ya wakazi 23543 ambapo wanaume ni 10,763 na wanawake ni 12780, kata ina vijiji 6 ambavyo ni Murukukumbo, Kabanga, Djululigwa, Ngundusi, Ibugana Nyabisindu, ina vitongoji 25 shule za msingi 7 za Serikali na shule 2 za watu binafsi, zipo shule 2 za sekondari ambazo ni Kabangana Nyabisindu, zahanati 3 na mahakama 1 ya Kabanga na kituo cha polisi kimoja ambacho hakijakamilika

Wakazi wa Kabanga wanajishughulisha na kilimo na ufugaji, na biashara, kuna misikiti 4 na makanisa ya kikristu 28, ipo minara ya simu ya TTCL na VODACOM

Miradi ya maendeleo iliyotekelezwa, ujenzi wa soko la kimataifa Nzaza-Kabanga mradi uko katika hatua za awali, ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na matundu 4 ya vyoo katika shule ya sekondari Nyabisindu majengo yapo katika hatua ya msingi, ujenzi wa maabara 3 Nyabisindu majengo yamekamilika.

Mapato na matumizi ya kata ya Kabanga, fedha zilizokusanya na ruzuku toka Serikalini kwa shule za msingi na Sekondari jumla kuu ilikuwa 136, 975,193.57/= matumizi kwa ujumla yalikuwa ni Tshs. 101,125,844.80/= salio lililobaki katika makusanyo na fedha za ruzuku lilikuwa ni Tshs. 35,849,348.52/=

**KATA YA NYAMIAGA**

Kata ya Nyamiaga ni moja ya kata zinazounda Wilaya ya Ngara, Kata hii ina vijiji 2 ambavyo ni Nyamiaga na Nterungwe. Kata ya Nyamiaga iko mbali wa km 3 kutoka makao makuu ya Wilaya, upande wa mashariki imepakana na Kata ya Rusumo, magharibi imepakana na Kata yaNgara mjini, Kaskazini imepakana na Kata ya Murukulazo na Kusini imepakana na Kata ya kibimba.

Vikao vya kisheria vilivyofanyika katika Kata ya Nyamiaga, Kamati ya Maendeleo ya Kata vilivyofanyika ni 3, hakikufanyika 1, Halmashauri ya maendeleo ya vijiji vilifanyika vikao 10, havikufanyika vikao 14, Vikao vya kitongoji vilifanyika vikao 32, havikufanyika vikao 88.

Kata ina jumla ya jumla 1,522 zenye watu wapatao 11,010 ambao kati ya hao wanaume ni 5023, na wanawake 5,637.

Hali ya ulinzi na usalama ni nzuri ambapo kata ina jumla ya wanamgambo 53

Shughuli za kiuchumi na kijamii katika kata ya Nyamiaga wakazi wanajishughulisha na kilimo, ufugaji na biashara ndogo ndogo.

Mapato na matumizi katika kata ya Nyamiaga, mapato yalikuwa ni Tshs. 2,290,000/= na matumizi yaliyofanyika ni Tshs. 1,847,000/= baki 443,000/=

Shule zilizoingia katika shule ya msingi Mumiterama mapato Tshs. 676,868.11/= na zilizotumika Tshs. 229,000/=, shule ya msingi Mugasha mapato Tshs. 685,971.03/= na zilizotumika Tshs. 411,400/= Shule ya msingi Kumuyange mapato ni Tshs. 739,223.00/= na zilizotumika 342,823.12/=

Miradi ya maendeleo katika Kata ya Nyamiaga, ujenzi wa maabara ya shule ya sekondari Nyamiaga msingi umekamilika, maandalizi ya ujenzi wa chumba cha darasa shule ya msingi Mumiterama kuna tripu 6 za mawe, ujenzi wa chuo cha ufundi stadi kuna tripu 26 za mawe, ukarabati wa jengo la masjala ambalo ndani yake kuna chumba cha ofisi cha Mtendaji wa Kijiji ukarabati umekamilika na jengo linatumika,ujenzi wa kisima cha maji katika kitongoji cha Nterungwe.

Kata ya Nyamiaga ina shule za msingi 3, zahanati 1, Baraza la Kata 1, Makanisa 12, Misikiti 2, Saccoss 1.

Uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la awali, Mumiterama wavulana 32 wasichana 25 jumla 57, Mugasha wavulana 43 wasichana 35 jumla 78, Kumuyange wavulana 23 na wasichana 38, wanafunzi wa darasa la 1, Mumiterama wavulana 60 wasichana 67 jumla 127, Mugasha wavulana 73 wasichana 54 jumla 127, Kumuyange wavulana 36 wasichana 38 jumla 74

Changamoto zilizopo katani, upungufu wa waalimu, utoro wa wanafuniz , ukosefu wa nyumba ya Mganga katika zahanati ya Nterungwe, ugonjwa wa unyanjano, kutokuwepo na ofisi ya serikali.

**KATA YA MUGANZA**

Kata iko kusini Mashariki mwa Wilaya ya Ngara na ni moja kati ya Kata 22 zinazounda Wilaya ya Ngara, Ina jumla ya wakazi 15616 ambapo wanaume ni 7555 na wanawake ni 8061 na kaya 3528, ina jumla ya vijiji 3 yaani Mukubu, Muganza na Mukalinzi, ina jumla ya vitongoji 19.

Kata ya Muganza ina viongozi wa kuchaguliwa kama ifuatavyo, Wenyeviti wa Serikali za vijiji 3, kati ya hao Chadema ni 1, nWenyeviti wa Vitongoji 19 kati ya hao Chadema ni 6 na Mheshimiwa Diwani 1.

Kata ina shule ya sekondari 1 inayoitwa Muganza Sekondari, Shughuli za kiuchumi ni kilimo na ufugaji, changamoto kwa mazao ni kushambuliwa na wadudu weusi waitwao battles

Kuna shule za msingi 8 ambazo ni Muganza, Ngeze, Rusengo, Mukubu, Nyakafandi, Rwimbogo, Musaza na Kuntatwemwa. Hali ya uandikishaji wa darasa la kwanza

waliandikishwa wavulana 475 na wasichana 402 jumla 877 pamoja na darasa la awali wavulana 272 na wasichana 259 jumla 531

Vyanzo vya mapato katika Kata ya Muganza ni soko la Mukubu na soko la mukalinzi ambalo lina wakala Bw. Suleiman Bunzia, jumla ya fedha zilizokusanywa mwezi Januari mpaka mwezi Aprili ni Tshs. 1,579,000/=

Vikao vya kisheria vilivyofanyika, Mukubu vilifanyika 3 vikao 6 havikufanyika, Mukubu vilifanyika 8 kikao 1 hakikufanyika, Mukalinzi vilifanyika 7 vikao 2 havikufanyika. Mikutano ya kijiji Muganza walifanya mkutano1 mikutano 2 haikufanyika, Mukubu ilifanyika mikutano 2 mkutano 1 haukufanyika, Mukalinzi ulifanyika mkutano 1, mikutano 2 haikufanyika. Mikutano ya Kamati ya Maendeleo ya Kata Muganza ilifanyika mikutano 3.

Miradi iliyotekelezwa katika Kata ya Muganza, ujenzi wa choo matundu 6 shule ya msingi, Ujenzi wa zahanati ya Muganza, ujenzi wa choo matundu 4 shule yamsingi mUganza bado mradi kuanza, ujenzi wa choo matundu 4 shule ya msingi Mukubu choo iko katika hatua ya mwisho ya kupaka rangi, ujenzi wa kibanda katika shule ya msingi kuntatemwa umeshaanza, ukarabati wa kisima cha maji kijiji cha Mukubu bado haujakamilika

Hali ya ujenzi wa maabara hadi sasa umefikia hatua ya ujenzi wa meza za ndani bado kuwekwa zege la juu kwa chumba cha kwanza na chumba cha pili bado meza 4

Hali ya ulinzi na usalama kwa kata ya Muganza ni nzuri kwani wananchi katika vijiji vyote wanafanya doria za usiku na viongozi wa vijiji wanasimamia zoezi hili la ulinzi na usalama kikamilifu.

Hali ya maambukizi ya ugonjwa wa VVU katika kata wapo wagonjwa ambao tayari wana maambukizi na tayari 2 walishatambulishwa ofisini, bado elimu inaendelea kutolewa kwa jamii ili waweze kujitokeza kwenda kupima afya zao.

**MUHT NA 22/2015/2016: MASWALI YA PAPO KWA PAPO**

Katibu alisoma maswali ya papo kwa papo na majibu yake kama ifuatavyo;

| Na. | **MUHUSIKA** | **SWALI** | **MAJIBU** |
|---|---|---|---|
| 1 | Mh. Philbert Kiiza, Kata ya Kasulo | Kituo cha Afya Lukole ni kimoja kati ya vituo vya | Kituo cha Afya Lukole ni kimoja kati ya vituo |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Afya 4 vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngara. Kituo hiki kipo km3 toka ulipo umeme wa TANESCO kupitia mpango wa umeme vijijini REA, kipo porini na kinahudumia watu wengi kutoka katika maeneo makubwa ya Kata ya kasulo, Rusumo, Nyakisasa na sehemu ya Wilaya ya Biharamulo lakini hakina miundo mbinu ya Nishati ya umeme.<br><br>Katika bajeti inayoendelea kwa sasa umeme utagharimu Tshs. 5,000,000/= ambazo hazijaletwa mpaka sasa, je Halmashauri ina mpango gani wa kupata kiasi hicho cha fedha kutoka katika vyanzo vyake vya mapato ya ndani na kuweka umeme badala ya kusubiri fedha hiyo kuletwa toka hazina? | vya Afya 4 vilivypo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ngara, Kituo hiki kupitia mpango wa umeme wa REA, kipo katika mpango wa kuwekewa umeme vijijini kupitia REA awamu ya tatu, hii inatokana na mpango wa REAWilayani Ngara walivyo baini kwa kufuata orodha ya majina ya vitongoji.<br><br>Kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Kituo cha Afya Lukole wamekiwekea bajeti ya kufanya wiring majengo yaliyoko kwenye kituo. |
| 2 | Mh. Nzeye Leonard, Kata ya Muganza | a) Shule ya Msingi Rwimbogo yenye vyumba 3 na ofisi viliezuliwa mwaka 2013 havikuwekwa kwenye bajeti | Ni kweli majengo ya shule ya msingi Rwimbogo madarasa 2 na ofisi viliezuliwa tarehe 06/01/2013, shule hiyo haikuweza kukarabatiwa kutokana na kutokuwepo mshikamano kati ya uongozi wa Kata na Serikali ya Kijiji wakati ule. Aidha hapakuwepo na fungu la ukarabati au |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | dharura kwenye bajeti za Halmashauri kama ilivyotokea kwenye shule ya msingi Murutabo, kukazuru na Mukagugo zilizopata maafa ya kuezuliwa pia.<br><br>Kuanzia sasa tathimini itafanyika upya kwa vile tathimini iliyofanyika tarehe 18/01/2016 ni ya muda mrefu na baada ya hapo Serikali ya Kijiji, Kata na Halmashauri zutaandaa utaratibu wa kukarabati madarasa hayo pamoja na shule zote zilizoezuliwa katika vipindi mbalimbali. |
| | | b) Barabara ya kutoka Mukalinzi kwenda Bitunga haikuwekwa kwenye bajeti | Barabara ya Mukalinzi-Bitunga yenye urefu wa km 7.0. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 barabara hii haikupitishwa kufanyiwa matengenezo kutokana na ufinyu wa bajeti, lakini kwa mwaka wa fedha 2016/2017 barabara hii tumeiweka kwenye bajeti kwa matengenezo ya kawaida |
| 3 | Mh. Wilbard Bambara, Kata ya Rusumo | Kwa kuwa k.9 kuna majengo ya kuanzia shule mpya ya msingi, kwanini tusitumie majengo haya yaliyokuwa ya REDESO kuanzisha shule ili kusaidia | Wazo la kuanzisha shule lina umuhimu sana na linakubalika katika eneo hilo kwa vile watoto wanatembea mwendo mrefu kwenda shule ya |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | watoto wadogo wanaotembea umbali mrefu zaidi ya km 7 hadi 10 kutafuta elimu ya msingi? | msingi Kasharazi na Kumunazi. Jambo la kufanyia kazi kwa sasa ni kuwaelekeza Wakaguzi wa shule, Mhandisi wa Ujenzi na Afisa Afya kufanyia tathimini majengo hayo ya REDESO kuona kama yanafaa kwa matumizi ya shule. Taarifa itawasilshwa kwenye kikao husika kwa maamuzi<br><br>Hata hivyo Halmashauri inasita kufungua shule mpya kwa vile shule zilizopo kwenye eneo hilo hazina miundo mbinu toshelezi ya wanafunzi waliopo mfano matundu ya vyoo, madarasa na nyumba za Waalimu . Waalimu wanapofundisha shule ya msingi Kasharazi wanaishi Kumuyange na majengo ya sogea. Aidha miundo mbinu hiyo inahitaji nguvu za wananchi walewale wa kijiji cha Kasharazi kuikamilisha. Kujengwa kwa shule hiyo kijiji cha Kasharazi kinatakiwa kuhudumia shule 3 yaani Kaburanzwili, Kasharazina hiyo ya k.9, huu ni mzigo mkubwa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | kwa wananchi. |
| 4 | Mh. Olipa A. Bugoke | Kata ya Mugoma ni miongoni mwa Kata zenye miradi ya maji, tangu mwaka 2012 mradi huo ulisimama kwa ajili ya kuharibika kwa pampu na pampu hiyo mpaka sasa iko mikononi mwa Halmashauri hivyo basi wananchi wa Kata ya Mugoma wanapenda kujua Halmashauri ina mpango gani juu ya ununuzi wa pampu hiyo na itapatikana lini? | Ununuzi wa mashine pamoja na pampu uliwekwa kwenye bajeti ya 2014/2015, fedha zilizopokelewa hazikutosha kununua mashine na kukabidhiwa katika ofisi ya kijiji.Ununuzi wa pampu upo kwenye bajeti ya mwaka 2015/2016 na pia tumeweka katika bajeti ya mwaka 2016/2017. Hata hivyo Halmashauri imeshaipeleka orodha ya miradi ya maji inayotakiwa kubadilishiwa teknolojia ya mashine zinazotumia dizel ili zifungiwe mitambo ya nishati ya umeme |
| | Mh. Olipa A. Bugoke | Kata ya Mugoma ni miongoni mwa Kata zilizo kwenye mpango wa kupewa mashine ya kukoboa kahawana kipindi hiki ndicho cha kuvuna kahawa na zimeiva sasa Halmashauri ina mkakati gani ili mashine hizo ziweze kupatikana | Katika mwaka wa fedha 2012/2013 Halmashauri ya Wilaya ilitenga jumla ya Tshs. 49,236,107 na kuongezea Tshs. 15,263,947 iliyofanya jumla ya fedha yote kuwa 64,500,054/=kwa ajili ya kusimika mashine za kukoboa kahawambivu katika Kata ya Mugoma. Ujenzi upo katika hatua za mwisho za ukamilishaji na kuifanyia majaribio. Wataalam wa bodi ya |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | kahawa Tanzania(TCB) watahusishwa katika kuifanyia majaribio ili iweze kukabidhiwa kwenye kijiji kwa ajili ya kuanza kutumika rasmi katika msimu huu |
| 5 | Mh. Catherine Edward | Mwaka jana niliomba kujua idadi ya vijiji/kata ambavyo vimetenga maeneo kwa ajili ya kulima wanawake na vijana nilijibiwa Baraza lijalo.<br><br>Nataka kujua ni vijiji vingapi vimetenga maeneo hayo, na kama bado naomba kujua utaratibu gani unaendelea kwa sababu wanawake na vijana wanasubiri wakabidhiwe mashamba hayo ili waanze maandalizi | Kwa mujibu wa takwimu kutoka Idara ya Maendeleo ya Jamii kitengo cha vijana, mpaka sasa ni jumla ya vijiji 15 tu vilivyotenga maeneo jumla ya ekari 418.5.<br><br>Katika kutekeleza agizo la Serikali la kuvitaka vijiji vitenge maeneo ya ardhi kwa ajili ya viwanda vidogo na shughuli za maendeleo ya vijana na wanawake, Halmashauri iliiwaandikia Watendaji wa Kata barua yenye Kumb Na. FA.991/9997/01/21 ya tarehe 14/08/2013 kuwaagiza wazijulishe Mamlaka ya vijiji kutenga maeneo ya ardhi kwa ajili ya makundi hayo. Aidha kupitia barua Kumb. Na.BE.139/284/01/E/102 ya tarehe 20/01/2016 kutoka Mkoani. Halmashauri imewaandikia Watendaji |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | wa Kata barua Kumb.Na. AC.453/824/01/79 ya tarehe 10/06/2016 na kuhimiza yatengwe maeneo ya viwandavidogo vijijini kwa ajili ya kuboresha maisha ya wananchi ikiwemovijana na wanawake<br><br>Vijiji hivyo ni kama ifuatavyo, Bugarama ekari 8, Rwinyana ekari 14, Kihinga ekari 20, Nyarulama ekari 14, Mumiramila ekari 60, Mkalinzi ekari 30, Mukubu ekari 35,Muganza ekari 10, Murutunda ekari 100, Nyabihamga ekari 70, Mumuhamba ekari 30, Murulama ekari 20, Kasulo ekari 5 Nyakiziba ekari 1, Murukulazo ekari 1.5 |
| | Mh. Catherine Edward | Kanuni ya Madiwani ilikuwa inaelekeza utaratibu wa vikao, Baraza wajumbe kupelekewa kabrasha siku 7 kabla, kwa Kamati za kudumu siku 3 kabla, je kanuni imebadilika na kama haijabadilika ni utaratibu upi inaomridhisha Mheshimiwa Diwani | Utaratibu haujabadilika kabrasha zitakuwa zinapelekwa kwa Waheshimiwa Madiwani kwa wakati kwa vikao vya baraza siku 7 kabla ya kikao. Kwa vikao vya kamati za kuduma kanuni ya 46(2) inasema kwamba taarifa ya vikao |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | kupokea kablasha | inatakiwa kuwafikia Waheshimiwa Madiwani angalau saa ishirini na nne yenye ajenda za kikao itabidikutolewa kwa Wajumbe kabla ya Mkutano. Hivyo utaratibu utazingatiwa |
| 6 | Mh. Rehema S. Ramadhani | a) Anataka kujua kuhusu choo ya soko la mjini kilichoboka miundo mbinu yake na kutoa harufu chafu hapo soko zima kimekwa kero kwa wananchi, kitakarabatiwa lini kuondoa kero hiyo<br><br>b) Kwa kuwa kituo cha afya Murusagamba kimekarabatiwa wodi 2 nataka kujua vitaletwa lini vifaa kama vitanda na magodoro ili wodi hizo ziweze kutumika kwa sababu wagonjwa hawana pa kulala naomba nipatiwe majibu iwezekanavyo<br><br>c) Nataka kujua makato yangu ya bima ya afya | Kuhusu ukarabati wa choo cha Ngara mjini sokoni, Idara ya Ujenzi tayari ilifanya makisio na kubaini gharama ya Tshs. 876,000/=, hivyo tunasubiri fedha ili kuweza kukamilisha matengenezo hayo.<br><br>Kituo cha Afya Murusagamba kimeishatuma maombi ya mkopo ya kununua magodoro 20 na vitanda 20 kutoka bima ya afya barua imepitishwa na Idara ya Afya kwenda Bima mkoa kufanyiwa upembuzi kama kituo kinaweza kulipa mkopo kwa wakati na kazi hiyo imekwisha kamilika na kutumwa bima taifa tuendelee kuwa na subira katika kukamilisha hatua za mwisho za mkopo<br><br>Hatua za kusajiliwa katika bima ya afya kwa kiasi Fulani huwa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | yanaenda wapi wakati siwezi kutibiwa kwenye vituo vya afya vya Wilaya yangu | zinachukua muda hata hivyo kwa suala hili limechukua muda mrefu zaidi Idara ya Afya imefanya Madiwani ili wafaidike na fedha yao inayokatwa kila mwezi jibu lake ni kwamba mteja anapougua na fomu yake imesajiliwa na bima ya afya anapaswa kupiga simu na kueleza mahali alipo na hali halisi ya uanachamawake hivyo hupewa namba maalumu ya kumuwezesha kutibiwa katika kituo chochote cha afya au hospitali mahali alipo. Hata hivyo baada ya kupitia nyaraka za Waheshimiwa Madiwani Wilaya ya Ngara hakuna malipo yoyote ya bima yaliyolipwa hivyo huduma hii haiwezi kutolewa mpaka utaratibu wa malipo ufanyike |
| 7 | Mh. Ndangwa F. Fridoline | Kuna taarifa zilizotolewa kwa Watendaji wa vijiji kuwa wazee wote wenye miaka 60 kwenda juu wapige picha kwa ajili ya msamaha wa matibabu, wazee wale wamefanya hivyo kata nzima ya Bugarama. Lakini kinachoendelea | Mpaka sasa Idara imesajiri wazee 2654 kiasi ambacho ni kidogo ukilinganisha na walengwa wanaotarajiwa kusajiliwa ambao ni 22280 sawa na asilimia 6% ya 371334 ambao ni jumla ya wakazi wa Ngara. Utaratibu huu |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | hakieleweki, je ni lini vitambulisho vya matibabu bure kwa wazee katika Kata ile vitatolewa? | wahuhakiki wazee wanao sitahili vitambulisho umeandaliwa kwa Kata zote 22 ikiwemo kata ya Bugarama hadi sasa majina haya yako kwa Afisa Ustawi wa Jamii ikiwa ni hatua za mwisho za uhakiki na baadae yatatumiwa kwa awamu, kwa Mganga Mkuu wa Wilaya kwa uhakiki wa mwisho na shughuli hii itakamilika katika kipindi cha wiki mbili hadi tatu. |

**MUHT NA 23/2015/2016: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA**

Wajumbe walifanya masahihisho yafuatayo;

- ***VyaVDCvilifanyika isomeke Vya VDC vilifanyika***
- ***Wapato isomeke wapatao***
- ***Inapaka isomeke inapakana***
- ***Kukaribisha isomeke Kumkaribisha***
- ***Imeundwana isomeke imeindwa na***
- ***Mji wa Ngara mdogo isomeke Mji mdogo wa Ngara***
- ***Tupeleke isomeke zipelekwe***
- ***Tamisemi isomeke TAMISEMI***
- ***Mukibungeye isomeke Mukibungere***
- ***Yatamilikisha isomeke yatamilikishwa***
- ***John Joseph Pombe Magufuli***

**MUHT NA 24/2015/2016: TAARIFA ZA KAMATI ZA KUDUMU**
**KAMATI YA FEDHA UTAWALA NA MIPANGO**

Mwenyekiti wa Kamati aliwasilisha taarifa, Wajumbe walipokea taarifa na kuipitisha, Mwenyekiti baada ya kuwasilisha aliwashukuru wajumbe kwa kupokea taarifa.

**KAMATI YA UJENZI UCHUMI NA MAZINGIRA**

Mwenyekiti wa kamati aliwasilisha taarifa ya na kueleza kwamba siku ya tarehe 21/04/2016, kamati ilipata barua toka TANESCO iliyoeleza maridhiano kati ya TANESCO na Serikali ya wananchi juu ya mradi wa ORIO Wilayani Ngara, aliomba Mkurugenzi Mtendaji kuwaandikia barua wanaohusika na kuwashukuru wajumbe. Wajumbe walipokea taarifa na kuipitisha.

**KAMATI YA ELIMU AFYA NA MAJI**

Mwenyekiti wa Kamati aliwasilisha taarifa. Wajumbe walipokea taarifa na kuipitisha na baadae aliwashukuru wajumbe kwa kupokea taarifa.

**KAMATI YA KUDHIBITI UKIMWI (CMAC)**

Mwenyekiti wa Kamati aliwasilsha taarifa, Wajumbe walipokea taarifa na kuipitisha na baadae aliwshukuru wajumbe.

**MUHT NA 24/2015/2016: TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO**

Afisa Mipango aliwasilisha taarifa. Wajumbe walipokea taarifa.

Mjumbe mmoja alitaka kufahamu ukurasa namba 44 Idara ya elimu sekondari taarifa iliyotolewa ni ya ujenzi wa vyoo na taarifa inazungumzia tena ununuzi wa vitabu.

Mjumbe mwingine alichangia ukurasa 45, utekelezaji wa ujenzi wa shule ya sekondari Murugwanza, aidha alizungumzia kwamba kama fedha zipo kasi ya ujenzi wa barabara ya Muhweza na Mukarehe na Bugoi ni ndogo, na barabara hizi hazifiki mwisho, alishauri Idara ya ujenzi badala ya kuweka kwenye Routine maintenance iwekwe katika matengenezo ya maeneo korofi.

Mjumbe mmoja alichangia kwamba ujenzi wa karavati kwenye barabara ya Mbuba-Ruhuba-Mkanyagali kipindi hiki cha mvua wanafunzi wanaokwenda shule ya msingi kumwendo wanapata shida kuvuka, aliomba ufanyike utaratibu wa kuweka daraja ambalo litasaidia watoto kuvuka.

Mwenyekiti alisisitiza ipi haja ya kufanya matengenezo katika eneo la Mkanyagali kwa sababu kuna wananchi wengi wanatumia barabara hiyo kwenda kupata huduma katika maeneo mbalimbali.

Mhandisi wa Ujenzi alijibu kwamba eneo la Mkanyagali, eneo hilo halipo kwenye mtandao, Idara ya ujenzi itaangalia makaravati yaliyopo na kuona namna watakavyosaidia kujenga karavati katika eneo la Mkanyagali

Wajumbe pia walijadili kuhusu taarifa ya mapato na matumizi kwamba hayalingani kwa sababu inaonekana fedha nyingi hazijatumika.

Mjumbe mwingine alisema kwamba miradi mingi ya SEDEP fedha zake hazijatumika ka wakandarasi hawajalipwa.
Katibu alijibu kwamba fedha za ruzuku za shule zilikuwa kwenye bajeti kabla ya waraka wa elimu bure kufikia mwezi Machi, fedha zilizotumika ni 43% ila kuna malipo yanaendelea kufanyika ambayo kwenye taarifa hii haijawekwa, fedha za SEDEP zipo na Wakandarasi hawadai fedha yoyote, Mkandarasi wa shule ya sekondari Murugwanza anasuasua ingawa waliomumba wafanye site meeting lakini bado kikao hakijafanyika na tatizo lipo kwa Mkandarasi.

**NENO TOKA KWA M/KITI WA CCM**
Mwenyekiti wa CCM aliwashukuru Wajumbe, na kusema kwamba Wataalam waandae taarifa mapema na kupeleka kwa mratibu wa vikao ili kuandaa vikao mapema na kuendana na kasi ya Mh. Rais wa awamu ya tano (5) wa Jamuhuri ya Muungano Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, pia uzabuni unaotolewa uangaliwe na kushauri kazi 2 zisitolewe kwa Mkandarasi mmoja kuepuka kufanya makosa. Alitoa taarifa ya makusanyo ya ushuru vijiji, aliwaomba Waheshimiwa Madiwani kusimamia ukusanyaji wa mapato, aidha alieleza pia ukosefu wa fedha kwa ajili ya malipo ya posho isiwe sababu ya kutofanyika kwa vikao vya Mamlaka ya mji mdogo Ngara na kumuomba Mh. Diwani wa Ngara Mjini asimamie suala hilo, Mkurugenzi Mtendaji ajitahidi kulipa madeni ya Wenyeviti wa Vitongoji.

Pia alizungumzia kwamba agenda kuhusu watumishi hewa iwe ya kudumu, na Mtumishi aliyekuwa anapokea mishahara 2 awajibishwe kwa sababu ameiibia Serikali, alipokea malalamiko mengi katika ofisi ya CCM kuwa wajane hawapati stahili zao inapotokea kufiwa na mke au mume hivyo ofisi ya Utumishi ijitahidi kuliangalia suala hilo kwa makini

**NENO TOKA KWA MKUU WA WILAYA**
Mkuu wa Wilaya aliwashukuru Waheshimiwa Madiwani kwa kushirikiana katika mapokezi ya ugeni wa Mheshimiwa Rais John Pombe Joseph Magufuli na pia ugeni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu khasim Majaliwa Majaliwa, aliomba ushirikiano na mshikamano huu uendelee, aidha alisema kwamba anafahamu kuna changamoto ya ujenzi wa maabara alisisitiza uwajibikajiili kukamilisha ujenzi wa maabara, matengenezo ya madawati Halmashauri kushirikiana na ofisi ya Mkuu wa Wilaya waliund kamati ambayo ilifanya harambee ya kuchangia madawati ili kuondokana na kero za madawati, aliwaomba Waheshimiwa Madiwani kufanya uhamasishaji ili wadau wote waweze kuhamasika na kuchangia.

Aidha alitoa taarifa kwamba Mwenge wa uhuru utapokelewa katika Kata ya Murusagamba tarehe 23/07/2016, alisema pia kwamba kulitokea mauaji katika kijiji cha Ibuga na kumpoteza mfanyabishara, alisisitiza katika mikutano ya vijiji kuhimiza Watendaji kutatua migogoro iliyokuwa katika maeneo yao.

**NENO TOKA KWA MH. JOHN SHIM I' IMANA**

Alianza kwa kuwashukuru wajumbe, Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi Mtendaji, aidha alieleza kwamba Waheshimiwa Madiwani wote wanatoka katika Chama cha Mapinduzi hivyo washikamane, Mkuu wa Wilaya ahakikishe mambo hayaendi mbali bila hajayashughulikia, alimuhakikishia Mkuu wa Wilaya na Mwenyekiti wa CCM kwamba walikuja kufanyakazi na kuendana na kasi ya Mh. Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Ndg. John Pombe Joseph Magufuli na Kata zilizoko katika Wilaya ya Ngara zibadilike na watawasimamia Watendaji wa Kata.

**MUHTA NA 25/2015/2016: KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe wote waliohudhuria kikao na uongozi wa CCM na kueleza yafuatayo

1. Walihudhuria kwenye kikao cha ALAT Taifa na kufanya uchaguzi na aliibuka mshindi, alieleza pia kwamba walipata changamoto wengine kutoyakubali matokeo, katika kikao Waziri Mkuu Ndg. Khasim Majaliwa Majaliwa alisisitiza kila Wilaya kukusanya mapato kwa 80% hivyo Waheshimiwa Madiwani wajiandae na kusimamia ukusanyaji wa mapato
2. Waziri Mkuu aliulizwa kuhusu mafunzo kwa Waheshimiwa Madiwani na alijibu kwamba utaratibu unaandaliwa ukishakamilika taarifa itatolewa, ilisisitizwa kwamba Mwenyekiti wa Halmashauri pamoja na Waheshimiwa Madiwani kuwa wasimamizi wakubwa kuhakikisha fedha haipotei, suala la ardhi limekuwa na changamoto kubwa baada ya Waziri Mkuu kufuta umiliki wa baadhi ya maeneo yaliyoachwa wazi kwa muda mrefu bila kuendelezwa na kila kijiji kinatakiwa kuwa na eneo lililoachwa wazi.
3. ALAT ni chombo cha kutetea Halmashauri hivyo maombi yaliyotolewa yatatolewa majibu katika kikao kitakachofanyika Musoma.

Alitoa pongezi kwa Mkuu wa Wilaya na uongozi wa Chama Cha Mapinduzi pia kwa Waheshimiwa Madiwani kwa kuichangia timu ya mpira ya Murusagamba, alisisitiza kwa wazabuni/ wakandarasi wanaoshindwa kumaliza kazi kutopewa kazi zingine na sheria ichukue mkondo wake, aliwasisitiza Waheshimiwa Madiwani kwenda Kabanga kwa ajili ya harambee ya kuchangia madawati. Kikao kilifungwa saa 8.01mchana .

**UMETHIBITISHWA**

**………….........    ……………………**
**Mh. Erick Nkilamachumu    Bw. Kevin S. Makonda**

**MWENYEKITI    KATIBU**

**Tarehe…………/…………..2016**